TANGAZO LA SERIKALI NA. 345 la tarehe 03/5/2024

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1))*

AMRI YA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA KIGOSI KUWA HIFADHI YA MSITU YA TAIFA KIGOSI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Eneo la Msitu wa Kigosi kuwa Hifadhi ya Msitu ya Taifa Kigosi ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Hifadhi ya Msitu ya Taifa Kigosi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA BIHARAMULO, BUKOMBE, MBOGWE, KAHAMA NA KALIUA

HIFADHI YA MSITU YA TAIFA KIGOSI


Makadirio ya eneo: Hekta 923904 au Kilometa za Mraba 9239.04.

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo la Ardhi ya matajiwazi, awali chini ya Eneo la Msitu wa Kigosi unaopatikana Wilaya ya Biharamulo, Bukombe, Mbogwe, Kahama na Kaliua katika Mkoa wa Kagera,

*Tangazo La Serikali Na. 345 (Linaendelea)*

Geita, Shinyanga na Tabora kama lilivyochorwa upya katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3182 (Skeli 1:250,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dodoma na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
25 Aprili, 2024

ANGELLAH J. KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*